GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)

Sehemu ya CXXVI Nam. 6661 **28 Julai, 2017** **Bei Shs. 1,000/=**

Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti *Hutolewa kila Ijumaa*

YALIYOMO Ukurasa

Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar Nam. 2 ya 2005.
Kanuni za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (marekebisho), 2017
(Chini ya Kifungu cha 44) 121

SEHEMU YA SHERIA

Tangazo la Sheria lililotajwa hapo chini limetangazwa katika ***Gazeti Rasmi*** hili.

Tangazo la Sheria

Nam. 60:- Kanuni za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar

SHERIA YA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR NAM. 2 YA 2005.

KANUNI ZA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR (MAREKEBISHO), 2017

MPANGILIO WA KANUNI

KANUNI **MAELEZO**

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Kusomwa pamoja na Kanuni Mama.
3. Kufuta na kuandika upya kanuni ya 10.
4. Marekebisho ya kanuni ya 12.
5. Marekebisho ya kanuni ya 15.
6. Kufuta na kuandika upya kanuni ya 16.
7. Marekebisho ya kanuni ya 25.
8. Kufuta na kuandika upya kanuni ya 59.
9. Marekebisho ya kanuni ya 69.

Matangazo yaliyohusu maiti, kuvunjikia kwa Ushirika na baadhi ya matangazo ambayo ni muhimu kwa watu kujua yanaweza kutiwa katika Gazeti. Nakala matangazo namna hiyo, zipelekwe kwa Mhariri wa Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Tanzania katika

TANGAZO NAM. 39

SHERIA YA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR NAM. 2 YA 2005.

KANUNI ZA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR (MAREKEBISHO), 2017 (Chini ya Kifungu cha 44)

KWA UWEZO niliyopewa chini ya kifungu cha 44 cha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar, **Mimi Dkt. KHALID SALUM MOHAMED,** Waziri wa Fedha na Mipango Zanzibar ninafanya marekebisho ya Kanuni za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar, 2017 kama ifuatavyo:

Jina fupi na kuanza kutumika.

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (Marekebisho), 2017 na zitaanza kutumika mara baada ya kuwekwa saini na Waziri na kutangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali.

Kusomwa pamoja na Kanuni Mama.

2. Kanuni hizi zitasomwa pamoja na Kanuni za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar, Tangazo Nam. 107 la 2007 ambazo katika Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni Mama.

Kufuta na kuandika upya kanuni ya 10.

3. Kanuni Mama zinarekebishwa, kwa kufuta kanuni ya 10 na kuiandika upya kama ifuatavyo:

"Muda wa malipo.

10.-(1) Michango yote ya mwanachama mwajiri na mwanachama mwajiriwa italipwa na mwajiri ndani ya siku kumi na tano baada ya mwisho wa mwezi ambao michango hiyo inahusika.

(2) Endapo mwanachama mwajiri atashindwa kuwasilisha michango ndani ya siku kumi na tano kama ilivyoelezwa chini ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, atalazimika kulipa adhabu ya aslimia tano (5%) ya kiwango cha jumla ya michango inayohusika".

Marekebisho ya kanuni ya 12.

4. Kanuni ya 12 (1) ya Kanuni Mama inarekebishwa kama ifuatavyo:

(a) kwa kufuta maneno "asilimia tano (5%)" yanayojitokeza katika aya ya (g) na kuweka badala yake maneno "asilimia saba (7%)";

(b) kwa kufuta maneno "asilimia kumi (10%)" yanayojitokeza katika aya ya (h) na kuweka badala yake maneno "asilimia kumi na tatu (13%)"; na

(c) kwa kufuta maneno "asilimia kumi na tano (15%)" yanayojitokeza katika aya ya (i) na kuweka badala yake maneno "asilimia ishirini (20%)".

Marekebisho ya

5. Kanuni ya 15(1) ya Kanuni Mama inarekebishwa kwa kufuta maneno "asilimia kumi na tano (15%)" baada ya maneno "atachangia Mfuko" na

6. Kanuni Mama zinarekebishwa kwa kufuta kanuni ya 16 na kuandika upya kama ifatavyo : Kufuta na kuandika upya kanuni ya 16.

"Maombi ya mafao". 16.-(1) Kwa mujibu wa Kanuni ya 23, mwanachama ataomba mafao yake kwa kujaza fomu maalumu na ataambatanisha hati maalumu za kuthibitisha mafao yake na atawasilisha fomu hizo katika Ofisi ya Mfuko.

(2) Mwanachama ambae atapata nyongeza ya utumishi na kuendelea kufanya kazi baada ya kutimiza umri wa lazima wa kustaafu, mafao ya mwanachama huyo yatalipwa baada ya kukamilika kwa kipindi cha muda wa nyongeza.

(3) Ukokotoaji wa mafao ya mwanachama aliyeongezewa muda wa utumishi utajumuisha pia na kipindi cha nyongeza katika utumishi.

7. Kanuni ya 25(1) ya Kanuni Mama inarekebishwa kwa kufuta maneno"muda wa miezi sitini ya kipindi cha mwisho" yanayojitokeza baina ya maneno "mshahara kwa" na maneno "kabla ya" na kuweka badala yake "miezi sitini (60) bora". Marekebisho ya kanuni ya 25.

8. Kanuni Mama zinarekebishwa kwa kufuta kanuni ya 59 na kuandika upya kama ifuatavyo: Kufuta na kuandika upya kanuni ya 59.

"Malipo ya pencheni na kiinua mgongo. 59.-(1) Mwanachama atakapofikia umri wa kustaafu na amechangia kwa miezi mia moja na hamsini na sita (156), atalipwa kiinua mgongo na pencheni kama ilivyoelezwa chini ya Jadweli la Kwanza la Sheria, na atalipwa pencheni kuanzia mwezi aliostaafu kazi na kwa miezi inayofuata.

(2) Endapo mwanachama hakutimiza muda wa miezi mia moja na hamsini na sita (156) ya kuchangia, atakapofikia umri wa kulipwa, atalipwa kiinua mgongo pungufu na pencheni pungufu kama ilivyoelezwa chini ya Jadweli la Kwanza la Sheria, na atalipwa pencheni pungufu kuanzia mwezi aliostaafu kazi na kwa miezi inayofuata.

9. Kanuni ya 69 ya Kanuni Mama inarekebishwa katika kanuni ndogo (4) kwa kufuta maneno"asilimia kumi na tano (15%)" yanayojitokeza katika aya (d) na kuweka badala yake "asilimia ishirini (20%)". Marekebisho ya kanuni ya 69.

IMETIWA SAINI leo 28 Juni, 2017.

(Dkt. KHALID SALUM MOHAMED)
Waziri wa Fedha na Mipango
Zanzibar